HISTORIA FUPI YA PAROKIA YA MTAKATIFU DOMINIKO SAVIO - MIKOROSHONI

JIMBO KUU LA DAR ES SALAAM

Parokia ya Mtakatifu Dominiko Savio Temeke Mikoroshoni, ni zao la Parokia ya Mtakatifu Francis Xavery Chang'ombe ikiwa ni miongoni mwa Parokia 154 zilizomo ndani ya Jimbo kuu la Dar es salaam na ni Parokia ya mia moja (100) kwa kuitamka kwa kinywa chake Mwadhama Baba Kadinali Polycap Pengo Askofu Mkuu Mstaafu mnamo tarehe 07 Julai 2016 kwenye sherehe ya Ibada ya Misa Takatifu ya Upadrisho katika Parokia ya Mtakatifu Petro Oysterbay..

Baada ya idadi ya waumini kuongezeka Parokia ya Chan'gombe, ilipelekea Parokia kuwa na Misa tano (5) kwa kila Dominika na pia umbali uliokuwepo kwa waumini wa Kanda za Vetenari na Mikoroshoni ambao uliwapelekea baadhi yao kutohudhuria Ibada za Misa Takatifu; hivyo basi Halmashauri ya Walei Parokia na Baba Paroko Steven Nyilawilawakati huo, walionelea ni vyema waanzishe Kigango maeneo ya Vetenari au Mikoroshoni.

Baada ya kiwanja cha Kanisa kupatikana kilibarikiwa mnamo 2004 na Mwadhama Polycap Kadinali Pengo chini ya uongozi wa Padre Andreas Komba

Chini ya uongozi wa Baba Paroko Padre Joseph Moshana Baba Padre George Sayi Paroko Msaidizi.

Kutokana na heshima ya Masista waliokuwepo wakati huo kukubali waumini wawe wanapata huduma kituoni kwao, Masista walipata heshima kutafuta jina la msimamizi wa Kigango miongoni mwa wanafunzi wa Mtakatifu Don Bosco; akapatikana Mt: Dominiko Savio ambaye alikufa akiwa bado kijana mdogo sana"

Ramani ya kanisa na nyumba ya Mapadre zimechorwa na muumini wa Parokia ya Chang'ombe ndugu Novat Ludovick kwa majitoleo

Ujenzi rasmi ulianza mwezi Februali 2010 chini ya uongozi wa Baba Padre Joseph Peter Mosha. Mkandarasi alikuwa muuminiwa Parokia ya Chang'ombe ndugu Samwel Salu -Salu and Company Ltd. Ujenzi huo ulichukua miaka tisa (9) kukamilika.

Jiwe la msingi liliwekwa na Balozi wa Baba Mtakatifu nchini Mhashamu Baba Askofu Joseph Chonet mnamo tarehe 04 Oktoba 2009. Mnamo mwaka 2009 kulifanyika mabadiliko ya uongozi; Baba Paroko Joseph Mosha alienda masomoni Italia na Baba Padre Benedict Shayo akaletwa kuwa Paroko

2012 Maadhimisho ya Sherehe ya Somo na Msimamizi wa Kigango yalifanyika, jozi 50 zilifunga ndoa siku hiyo.

Mnamo tarehe 19 Septema 2014 Kipaimara kilitolewa Kigangoni kwa mara ya kwanza na Monsinyori Deogratias Mbiku na mara ya pili ni Mhashamu Askofu Augustino Shao Askofu wa Jimbo la Zanzibar kwa niaba ya Baba Mwadhama

Mnamo tarehe 06 Januari 2016 kwenye Ibada ya Misa Takatifu ya Ushemasi,Mhashamu Eusebius Nzigilwa alivitangaza Vigango11 kuwa Parokia Teule Mikoroshoni ikiwemo.

Mnamo tarehe 07 Julai 2016 katika Misa Takatifu ya Upadirisho iliyofanyika Parokia ya Oysterbay, Mwadhama Kadinali Polycap Pengo aliitangaza Parokia yetu Teule kuwa Parokia kamili ya mia moja(100) Padre Canisius Adam Hali kuwa Paroko wa kwanza wa Mikoroshoni.

Mnamo tarehe 06 Mei 2018 Sikukuu ya Somo na Msimamizi wa Parokia yetu Kanisa lilibarikiwa na kuzinduliwa, Sakramenti ya Kipaimara ilitolewa, Baba Paroko alisimikwa na kubariki kiwanja cha ujenzi wa nyumba ya Mapadre na Baba Mwadhama Kadinali Pengo.

Vyama vya kitume

UWAKA, WAWATA, VIWAWA, Utoto Mtakatifu, UKWAKATA, Karismatiki, Utume wa Fatima, Watumishi wa Altre (Ministrant)